Kikundi kinachowafanvia

Voices of Youth www.unicef.org/voy/

Toleo la ripoti ya wataalam wa mikutano kwa vijana kuhusu utokomezaji wa aina zote za ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya watoto wa kike.

Acha ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya wasichana.

Unaweza kufanya kitu

Kabla ya kuanza…

Kabla ya kuanza kusoma makala haya jinsi wataalam wanavyofikiri ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya watoto wa kike vitazuiwaje, tungependa ujibu swali:

Endapo ungekuwa Raisi wa nchi kwa siku moja, ungewafanyia nini watoto wa kike?

Sasa…

Hebu soma ujifunze wataalam nao wanafikiri nini….na kisha ujibu maswali mwishoni mwa kila sehemu utuelezee nini kifanyike. Tutumie majibu yako kabla ya tarehe **15 Januari 2007**. Unaweza kututumia majibu yako kupitia njia yoyote kati ya hizi 3:

- **Tovuti**: Sauti za Vijana(http://www.unicef.org/voy/) kisha ingia "Zuia ubaguzi na ukandamizaji dhidi ya wasichana" ili ujibu maswali yaliyoko kwenye mtandao.
- **Barua pepe**: voy@unicef.org, pamoja na kichwa cha habari "Acha Ubaguzi na ukandamizaji dhidi ya wasichana".
- **Kwa Barua**: Voices of Youth, 3 UN Plaza, New York City, NY 10017, USA.

ISTILAHI

Ufuatao ni ufafanuzi mfupi wa baadhi ya maneno na misemo itakayojitokeza kwenye ripoti. Itabeba alama hii 🕮 hivyo utaitambua kirahisi.

Taasisi Mama

CSW: Kamisheni ya Hadhi ya Wanawake – Tawi la Umoja wa Mataifa linalounda kanuni za kuinua haki za wanawake.

DAW: Divisheni ya Maendeleo ya Wanawake – hili ni tawi la Umoja wa Mataifa linaloiratibu CWS.

UN: Umoja wa Mataifa – Shirika la Kimataifa lililoundwa 1945 kuyaleta pamoja mataifa yote ulimwenguni ili kufanya kazi ya kuleta amani na maendeleo, ikizingatia haki, hadhi, na ustawi wa watu wote.

UNICEF: Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa – Tawi la UN linaloshughulikia kuinua haki ya kuishi, haki ya kulindwa, maendeleo na ushirikishwaji wa watoto wote.

Mikataba Muhimu ya Kimataifa

CEDAW: Kongamano juu ya utokomezaji wa aina zote za uzalilishaji dhidi ya wanawake – mkataba uliosainiwa na nchi nyingi unaoainisha ugandamizaji dhidi ya wanawake na kuweka mikakati wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa na taifa.

CRC: Kungamano juu ya Haki za Mtoto – mkataba unaoweka bayana haki za kisheria kwa watoto wote (umri 8 – 10), ikijumuisha haki ya kupata elimu afya habari ushirikishwaji, maarifa na fursa ya kukua na kustawi. Mkataba huu umesainiwa na karibu nchi zote duniani.

Misamiati na Misemo:

Ubaguzi – pale mtu anapotendewa isivyo sababu tu ya rangi, jinsia au dini yake.

Kuwezeshwa – ni kitendo cha kumruhusu mtu kutawala maisha yake kimaamuzi kwa kujifunza, kuwa na vitendea kazi, kufahamu pamoja na nafasi ambayo hakuna mtu awezaye kumpokonya.

Unyonyaji – kitendo cha kumtumia mwenzako kwa faida yako, kwa ubinafsi wako na kijinufaisha kwa gharama zao.

Ukeketaji – unahusu hatua zote zinazoendana na mila na desturi ambazo huondoa kasehemu au kiungo chote cha uzazi cha msichana au mwanamke.

Ujinsia – Inamaanisha sifa na tabia zinazotarajiwa na jamii kwa mwanamke au mwanaume, msichana au mvulana. Ujinsia unatofauti na jinsia ambayo inamaanisha baiolojia ya msichana na mvulana, wanawake na wanaume.

Usawa wa jinsia – imani kwamba watu wote, iwe wasichana ama wavulana, wanawake au wanaume, wana thamani na haki sawa na lazima wawe na fursa sawa.

VVU – virusi(Virusi Vya Ukimwi) vinavyodhoofisha kinga ya mwili dhidi ya maradhi. VVU husambazwa kupitia ngono zembe au kushirikiana sindano. Mtu anaweza kuishi na VVU kwa muda mrefu akiwa na afya yake.

VVU/UKIMWI – VVU vyaweza kugeuka na kuwa UKIMWI (Upungufu wa Kinga Mwilini). Bila matibabu sahihi UKIMWI unaweza, na hakika unaua watu wengi. Katika nchi nyingi ama yanatolewa matibabu hafifu au hayapatikani kabisa kwa watu wanaoishi na UKIMWI.

Haki za binadamu – sheria ya kimataifa inakubaliana kwamba binadamu yeyote bila kujali rangi, utamaduni, jinsia, dini ama umbile lake, anahaki ya msingi kutendewa kwa uungwana bila ukatili.

Ukiukaji wa Haki za Binadamu – vitendo, tabia au maneno machafu ambayo huvunja haki ya msingi ya binadamu. Ukiukaji huu ni haramu na unavunja sheria za kimataifa.

Mkimbizi wa Ndani (IDP) – Huyu ni mtu alielazimika kuhama na kuacha makazi yake kwa sababu za uvujwaji wa haki za kibinadamu ama sababu za kivita. Mtu huyu hajaihama nchi yake kwenda nchi nyingine.

Wasichana Wasagaji – wasichana ambao huvutika kimaumbile na kimapenzi kwa wasichana wenzao.

Wanasihi – Watu wazima (wazee) ambao wanaweza kutoa ushauri na miongozo kwa vijana**.**

Asasi Zisizo za Kiserikali (NGO) – mashirika ambayo hayahusiani na serikali. Haya hufanya kazi ya kuwalinda na kuwasaidia wenye mahitaji katika jamii.

Wahamaji – jamii ya watu wanaohamahama badala ya kuweka makazi sehemu moja.

Desturi – kipimo cha tabia kinachozingatiwa na jamii na tamaduni.

Kistuula – matatizo ya kiafya ambapo kishimo hujitokeza kati ya uke na mkundu (nyuma), na kumfanya msichana kutokwa ovyo na mikojo.

Kundi rika – watu wa rika moja au msimamo mmoja.

Elimu Rika – elimu kupitia mwingiliano kati ya kundi la watu wa rika na hadhi sawa, kwa mfano kuongea na marafiki kujifunza kuhusu VVU na Ukimwi.

Umalaya – wakati mtu anafanya ngono au kushiriki katika matendo ya ngono na mtu mwingine kwa malipo ya pesa, upendeleo ama aina yoyote ya malipo.

Mkimbizi – mtu alielazimika kuacha makazi yake kwa sababu ya uvunjaji wa haki za binadamu au vita. Kwa sababu wanakosa ulinzi na usalama nchini kwao,wakimbizi huondoka na kuhamia nchi nyingine.

Ugandamizaji – kitendo chochote au maneno yanayodhamiriwa ili kusababisha jeraha au madhara kwa wengine.

"Watoto waliokosa mahitaji yakimsingi ya maisha wanatumiwa...wananyonywa katika mikono ya watu kwa namna nyingi wakiachwa kwenye hofu bila msaada wowote kwenye hatari kubwa."

- msichana, miaka 19, Umoja wa falme za Kiarabu (UAE)

UTANGULIZI

Taasisi ya hadhi za Wanawake ni nini?

📖Taasisi ya hadhi za wanawake (CSW) ilianzishwa mwaka 1946 na hukutana kila mwaka kuandaa mapendekezo na ripoti kwa 📖Umoja wa Mataifa. CSW inapania kuinua haki za wanawake ili kupata haki sawa kwa wanawake na wanaume, wasichana na wavulana. Mwaka huu, nchi wanachama wa CWS watakutana kuanzia Februari – Machi 2007 kuzingatia "Utokomezaji wa aina zote za 📖ubaguzi na 📖ugandamizaji dhidi ya mtoto wa kike." Ubaguzi unamaanisha pale mtu anapotendewa kinyume kwa ajili tu ya rangi, 📖jinsia, au dini yake. Ubaguzi mara nyingi hupelekea ugandamizaji.

Ripoti ya Wataalamu

Mnamo Septemba 2006, mjini Florence, Italia, kundi la wataalam kuhusu hali za watoto wa kike duniani kote, lilikutana kuandika ripoti ya jinsi wanavyofikiri nini dunia na viongozi wake wafanye kuhusu watoto wa kike. Ripoti yao itawasilishwa CSW mwaka 2007 kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa New York na itatumika kutaarifu majadiliano na mapendekezo ya mwisho kwa serikali wanachama.

Kwanini toleo la ripoti ya wataalam kwa vijana?

Dhumuni hasa la toleo hili la ripoti ya wataalam kwa vijana ni kukupa wewe nafasi ya kuguswa kwa kile wataalam wanachosema. Sauti yako na sauti ya vijana duniani pote, hasa watoto wa kike wa vijijini au sehemu zenye matatizo, zitasikika kwa mwitiko wa matatizo ya ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya watoto wa kike. Mapendekezo au ushauri utakaotoa vitajumuishwa kwenye muitikio wa vijana utakao wasilishwa kwenye tukio hili muhimu la Umoja wa Mataifa.

Nini kilichopo kwenye hiyo ripoti ya wataalamu?

Katika kila sehemu ya toleo la ripoti ya vijana utapata maelezo ya jambo fulani, nini wataalam wanasema kuhusu jambo hilo, baadhi ya mambo ya ukweli ya kukufikirisha, na maswali mawili ya kujadili na kutolea majibu. Masuali hayo mawili yanayopatikana mwishoni mwa kila fungu yatakuuliza nini kimekosekana ndani ya ripoti na ni nini kifanyike kupata ufumbuzi ya matatizo yaliyotajwa.

Unaposoma, Jaribu kuona na kufikiri kitu chochote ambacho kitakuwa kinaachwa au kusahauliwa na wataalam. Unajua hali yako zaidi ya yeyote yule! Unaweza pia kufikiri nini kifanyike kutatua matatizo yaliotajwa na ni nani awajibike kutenda kazi hiyo. Elewa kwamba wapo watu wengi wanaoweza kusaidia, ukijumuisha wazazi, walezi, wasimamizi, walinzi, waalimu, viongozi wa dini, polisi, watoa hudumu za afya, wauguzi, madaktari, wanasheria, wanasiasa, 🕮NGO, maserikali, Umoja wa Mataifa na watoto wengine na vijana.

Je mapendekezo yangu yataathiri matokeo?

Unaweza usiamini jinsi mapendekezo yako yatakavyoweza kuleta matokeo. Tazama huu mchoro chini uone jinsi mapendekezo yako yanavyoweza kuwa sheria au kanuni:



I. SHERIA NA SERA

KUVIWEKA KATIKA MATENDO

Huenda umeshawahi 🕮kubaguliwa na 🕮kugandamizwa bila sababu zaidi tu kuwa wewe ni mtoto wa kike. Hali hii inaendeleaje wakati watu na mara nyingine hata polisi wanaangalia? Je hakuna sheria zinazoharamisha hii kitu?

Kwa hakika zipo sheria zinazokulinda dhidi ya ubaguzi na ugandamizaji; na hii ni haki yako. Na ni wajibu wa serikali yako kuona sheria hizi zinatekelezwa.

Karibu nchi zote duniani zimejitoa kimasomaso kuhakikisha watoto wote – wake kwa waume, wanapata haki ya kuishi, kukua, ulinzi na kushirikishwa. Hii inajumuisha haki ya kupata elimu, matibabu, maarifa, ustadi, fursa ya kukua na kustawi, fursa ya kueleza maoni yake, haki ya kusikilizwa na haki ya kuishi huru bila kubaguliwa. Nchi zimeonyesha jinsi zilivyojitosa kuhakikiksha haki hizi zinalindwa kwa kusaini mikataba ya kimataifa kama vile Sheria ya Haki za Watoto (CRC) na 🕮Sheria Kufuta aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW). Kwa kusaini mikataba hii, kila serikali inachukua jukumu la kutunga sheria za kitaifa na sera zitakazotekeleza haki hizi.

Lakini ni kitu kimoja kuweka ahadi kwenye makao makuu ya 🕮Umoja wa Mataifa New York, na kisha ni kitu kingine kuhakikisha ahadi hizi zinakulinda wewe na watoto wote wa kike duniani. Kwa bahati mbaya, nchi nyingine zina uelewa tofauti wa nini haswa maana ya haki za watoto, watoto wa kike na
🕮Haki za Binadamu, na kwahiyo hawawalindi watoto wa kike kama ilivyokusudiwa kwenye mikataba.

Katika nchi nyingi, sheria za kitaifa hazifiki kwenye baadhi ya jamii nyingi kwa sababu ya kukosekana kwa vyombo vya dola sehemu hizo, kama vile mahakama na polisi, na uvunjaji wa haki za binadamu bado upo kwenye “sehemu zilizojificha” ndani ya familia au jamii.

Uvunjwaji wa haki za Binadamu umejadiliwa katika ripoti ya wataalamu kama ifuatavyo:

- **Upendeleo kwa mtoto wa kiume –** kwa kuwa tamaduni nyingi huthamini zaidi mtoto wa kiume kuliko wa kike, wasichana wengi hawapati hata nafasi ya kuzaliwa na hata hao wanaozaliwa hawapati kiuhakika chakula, malazi, elimu na matibabu kama wenzao wavulana.
- **Mtoto na Ndoa za kulazimishwa –** wasichana wengi wanalazimishwa kuolewa na kunajisiwa wangali bado watoto wadogo sana.
- **VVU na UKIMWI –** wasichana wanaathirika zaidi na 🕮VVU na UKIMWI kuliko wavulana kwa sababu hawana uwezo wa kujikinga wenyewe na virusi hatari ama hawawezi kupata matibabu yake.
- **Uwepo wa mila potofu –** familia na jamii nyingi bado zinaendeleza mila za zamani ambazo zimethibitika kuwa na madhara makubwa sana kwa wasichana, kama vile ndoa za utotoni na 🕮ukeketaji.
- **Hali ya migogoro –** mara nyingi watoto wa kike wamekuwa wakiandikishwa na kufunzwa matumizi ya silaha kama wanajeshi watoto, ama wamekuwa shabaha ya ukatili na kubakwa kunako migogoro.
- **Unyonyaji🕮 kwa wasichana kutumikishwa katika ukahaba –** Wasichana wengi wanalazimishwa kuingia kwenye 🕮Umalaya na kwenye ajira mbaya za watoto - muda mrefu hata kabla hawajakomaa kiakili na maungo na kabla maumbile yao hayajawa tayari kwa kujamiiana na kazi za sulba.
- **Mzigo wa kazi "za kike" –** mara nyingi wasichana wanategemea kusaidia shughuli za majumabani mwao na wakati huo huo kutafuta kipato kwa kufanya kazi kwenye nyumba za familia nyingine. Hivyo, watoto hawa wanapata muda mchache sana na fursa haba ya kucheza, elimu na kujiendeleza.

Tafakari
Ikiwa utaolewa kabla ya kutimiza umri wa miak 18, je unafikiri utaweza kupata fursa sawa kwenye elimu na kufikia malengo yako kweli kuliko ungeliolewa

Mapendekezo ya wataalam

Kuna kazi kubwa ya kufanywa na kila mmoja wetu, haswa serikali na Asasi Zisizo za Kiserikali zifanyazo kazi katika nyanja ya haki za binadamu na sheria za kimataifa. Mara nyingi, serikali huchukua hatua pale tu wanapobanwa na wananchi wao na vikundi

vya jamii. Baadhi ya mapendekezo yaliyoorodheshwa kwenye dondoo za wataalam ni:

- watu zaidi na zaidi wanapaswa kuelewa kuhusu makongamano (CRS na CEDAW) yanayolinda haki za watoto na wanawake. Hii itawezekana endapo serikali zitatoa msukumo wa Elimu kuhusu haki hizi kwa familia na jamii nzima.
- Sheria na sera za kimataifa vyapaswa kulenga sawia kwenye haki na mahitaji ya watoto wa kike na kuwa thabiti na mikataba ya kimataifa iliyosainiwa na hizo serikali.
- Sheria za taifa zinapaswa zilingane na zile za kimataifa kwenye masuala ya haki za wasichana na sheria zote zinazowabagua wasichana lazima ziondolewe.
- Vyombo vya dola (kama polisi) wakala wa sheria (mahakama) na mashirika ya ndani yanapaswa kupatiwa mafunzo ya jinsi ya kuchukua hatua punde ukiukwaji unapotokea ndani ya familia na jamii.
- Wakati serikali zinapowasilisha taarifa kwenye Umoja wa Mataifa zinapaswa pia kutakiwa kutoa taarifa zao juu ya hali za watoto wa kike.

> ***"Kila siku karibu kila sehemu ya India kasichana kanabakwa ndani ya vyombo vya usafiri ama kananajisiwa kwenye maduka ya jumla na hata masokoni – mbele ya watu wanaokaa kimya tu bila kufanya chochote. Hata mapolisi nao wanawatusi waathiriwa na familia zao." - msichana*, umri 16, India**

? Maswali ya kuyafikiria na kuyajibu

- Chunguza orodha ya uvunjwaji wa haki za binadamu, unafikiri chochote kimekosekana kwenye orodha hiyo? Kama kipo, wewe ungeongezea nini na kwa nini unafikiri yana umuhimu?
- Nini kifanyike kuhakikisha sheria na sera zinawekwa kwenye matendo na ni nani anapaswa awajibike kuona haya yanafanyika?

II. UBAGUZI

KUTAMBUA NA KUPANMBANA NA UKOSEKANAJI WA USAWA BAINA YA WASICHANA NA WAVULANA

Unapokua, unaweza kukabiliana na matarajio nini unapaswa kufanya na maisha yako. Unaweza kutarajia kusaidia kazi za nyumbani, kuwaachia wavulana na wanaume wakufanyie maamuzi, kufanya ngono, kuolewa na kuzaa watoto ungali bado mdogo bila kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi ya mustakabali wa maisha yako mwenyewe. Hautegemewi kusema "hapana" pale wanaume wanapokutaka kwa kitu fulani. Kwanini hali hii bado ipo sehemu nyingi duniani hadi leo?

Ukweli: Watoto mil,115 pote duniani hawapo shule za msingi – zaidi ya nusu yao ni wasichana.

📖Kanuni jinsia na muundo jinsia ni sababu kuu za 📖Ubaguzi na 📖Ugandamizaji wanazokabiliana nazo wasichana wengi. Matarajio ya wasichana yalioainishwa hapo juu yamekuwa sehemu ya maisha ya jamii kwa muda mrefu na yamekubalika kama 📖kanuni kwenye jamii nyingi. Zipo sababu nyingi kwanini kanuni na miundo jinsia inakuwepo, kati ya sababu hizo ni:

- **Uhaba wa fursa ya kumiliki –** Sheria zilizopo katika baadhi ya nchi inafanya iwe vigumu kwa wasichana wengi na wanawake kumiliki mali zao wenyewe, na kupata pesa ama urithi toka kwa wazazi wao. Bila kipato, wasichana wengi wanalazimika kuwategemea wanaume katika maisha yao.
- **Utamaduni na dini –** Mara nyingine matarajio tuliyonayo kwa wasichana ni yale yaliyojikita kwenye dini na mila, na hivyo kuwia vigumu kuzibadili, haswa pale zinapoungwa mkono na sheria mahalia.
- **Kuwatizama wasichana kama chombo –** Wasichana, hata katika umri mdogo sana, wamekuwa mara nyingi wakionekana kama vyombo, kuliko kama binadamu. Matokeo yake, wamekuwa wakitafutiwa soko na kuuzwa kama bidha.

Tafakari
Kwa nini unafikiri wapo wavulana wengi zaidi mashuleni kuliko wasichana?

- **"Sehemu zilizojificha" –** Ubaguzi na ugandamizaji umekuwa ukitokea ndani kwa ndani katika familia na jamii, pahali ambapo hapagunduliki kirahisi na watu ambao wataweza kusaidia. Watu wamekuwa wakihisi si juu yao kujiingiza kwenye masuala ya familia nyingine.

Mapendekezo ya wataalamu

Unaweza kufikiri hakuna la ziada linaloweza kufanyika kuhusu matazamio na desturi zilizodumu kwa muda mrefu kiasi hicho, lakini kipo.

- Tunapaswa kuwasaidia watu kuongelea kwa uwazi kuhusu 🕮kanuni jinsia na majukumu yanayopelekea 🕮ubaguzi na ugandamizaji.
- Lazima tufanye kazi ya kumwelimisha kila mmoja - wasichana, wavulana, wakinamama, wakinababa, walezi, viongozi wa dini, walimu, viongozi wa jamii, madaktari, manesi, wanasheria – kuhusu haki za wasichana, na kuwahimiza pia kuwasaidia kuchukua hatua dhidi ya ubaguzi.
- Lazima tuwapate viongozi wa jamii (kama mapadri, wanasiasa au waalimu), hasa wanaume na wavulana ambao watajiunga na wanawake na wasichana kwamba kila mmoja anapata haki na fursa sawa.

"Katika nchi nyingi, wasichana hupewa chakula kidogo kuliko wavulana. Pia wasichana hupewa lishe duni kuliko kaka zao. Na kwa sababu wasichana wanaweza kupata huduma duni za afya kuliko wavulana, lishe duni kwa wasichana yaweza isigundulike hata kupelekea matatizo makubwa ya kiafya…" – msichana, umri 20, Jamhuri ya Korea

- Hatuwezi kuogopa kuingilia kati na huhoji kanuni jinsia ndani ya familia ambayo haki za mtoto wa kike zinavurugwa.

? Maswali ya kuyafikiria na kuyajibu:

- Angalia orodha ya chanzo cha ubaguzi na ukatili. Unadhani kuna kitu kimekosekana? Kama kipo, ni kipi na kwa nini unadhani ni muhimu?
- Kifanyike nini kukomesha ubaguzi na ukatili dhidi ya watoto wa kike na ni wajibu wa nani?

III. WASICHANA WASIOONWA

KUWATAFUTA NA KUWALINDA WATOTO WA KIKE WALIOFICHIKA NA KUSAHAULIKA

Jifikirie kama ungekuwa huonekani. Ingekuwaje kama hakuna mmoja anayekujali au kukusikiliza unapoongea mahitaji yako na hakuna anayeyatilia maanani? Labda hulazimiki kudhania hivi kabisa. Labda huu ni ukweli kwako kama ilivyo kwa wasichana wengi duniani leo hii. Huenda pia unahitaji sana msaada na huwezi kuupata, labda "hauonekani".

Ukweli: Katika Afrika (kusini mwa jangwa la Sahara) asilimia 75 ya waathirika wapya wa VVU ni wasichana na wanawake wenye umri mdogo baina ya 15 na 24..

Watoto wa kike wasioonekana hawalindwi na sera wala programu zilizopo. Mara nyingi wanakuwapo kwenye sehemu zilizo ngumu kufikika (vijijini, nchi zilizoharibiwa na vita) ama wanafanywa wazionee haya hali zao na hivyo wanaogopa kuongea kuhusu matatizo yao. Wasichana hawa wasioonekana hatimae hukua na kuwa wanawake wasioonwa. Wakati kuna wasichana wengi katika hali hii, ripoti ya wataalamu inatambulisha makundi yafuatayo ya wasichana wasionekana:

Tafakari
Kwa nini unadhani wasichana wako kwenye hatari zaidi ya kuambukizwa VVU kuliko wavulana?

- Wasichana waliombukizwa ama kuathiriwa na VVU na UKIMWI
- Wasichana wanaojamiiana lakini hawawezi kupata huduma za afya
- Wasichana wenye ulemavu
- Wasichana 🕮wanaokeketwa
- Wasichana wanoteseka na 🕮kistula
- Wasichana wanaoolewa
- Wasichana mama wa nyumbani
- Wasichana wanaodhalilishwa au kubakwa
- Wasichana 🕮wanaonyonywa
- Wasichana wanaolazimishwa kuolewa na majeshi yanayopigana
- Wasichana wenye majukumu kama wazazi, kutunza nyumba, watafuta riziki na walinzi wa wadogo zao
- Wasichana wanaofanyishwa kazi za nyumbani.
- Wasichana wanaouzwa utumwani
- Wasichana wanaousishwa na pande zinazopigana
- Wasichana 🕮wahamaji
- Wasichana 🕮Wakimbizi au 🕮Wakimbizi wa ndani
- Wasichana walio magerezani
- Wasichana 🕮wasagaji

Mapendekezo ya wataalamu

Tumegundua namna ya kuwatambua wasichana wenye matatizo pamoja na jinsi ya kuwasaidia watoke kwenye hali ngumu inayowakabili. Vile vile tunalazimika kuhakikisha kwamba wasichana hawa wanashiriki kikamilifu katika maamuzi yanayoathiri moja kwa moja maisha yao ya baadae. Ripoti ya wataalamu inapendekeza namna sifuatazo za kuwatambua na kuwalinda wasichana wanaokabiliwa na matatizo mbali mbali:

"Mimi nafanya kazi zote za ndani... Napika chakula na kuosha vyombo. [Kaka yangu] yeye anakula na kucheza tu." – binti, mwenye umri wa miaka 10, Ethiopia

- Ni lazima kuwe na utafiti zaidi kuhusu wasichana wenye shida ili tuweze kufahamu walipo, ni kina nani na wanahitaji nini.
- Ni lazima kuwe na mipango ya kutatua matatizo ya wasichana wenye shida – mipango inayoweza kuwafikia katika jamii zao, kuwatafuta ili kuwasaidia hata kama hawaonekani.
- Ni lazima kuwa na njia nzuri za kuangalia kama mipango ya kuwasaidia wasichana wenye matatizo inawasaidia hasa walengwa hawa (yaani uratibu na ukaguzi).

? Maswali ya kuyafikiria na kujibu:

- Tazama orodha ya wasichana wenye shida. Unadhani kuna makundi yanayokosekana? Kama yapo, wewe ungeyaongeza yepi na kwanini unafikiri ni muhumu kufanya hivyo?
- Viongozi wa kijamii, vijana na wengineo wanawezaje kutafuta njia bora ya kuwalinda wasichana? Nani anapaswa kuhakikisha kuwa wasichana wanapata haki zao? Nani anapaswa kuwasaidia wasichana wenye shida?

IV. KUWEZESHWA

UTAWALE MAISHA YAKO

Kuwezeshwa ni nini? Inawezekana umesikia watu kwa nyakati na sehemu mbalimbali wakisema wawezeshe. Kuwezesha ni kitendo cha kumruhusu mtu kutawala maisha yake kimaamuzi kwa kujfunza, kuwa na vitendea kazi, kufahamu pamoja na nafasi ambayo hakuna mtu awezaye kumpokonya. Watu wanaokuzunguka, kama vile marafiki, wazazi, walimu na wengineo wanaweza kukupa mamlaka. Ukipewa mamlaka, unapata nafasi nzuri ya kufanya maamuzi kuhusu maisha yako, na utaweza kujilinda dhidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu.

Ukweli: Katika Asia, wasichana wasiopungua milioni 60 'hawaonekani' kutokana na wazazi wanahakikisha hawazaliwi na kukua – kwa sababu tu ni wasichana.

Vile vile unaweza kunyimwa mamlaka kama unaishi kwenye mazingira hatari na magumu. Ni muhimu kupambana na ubaguzi wa kijinsia unaowanyima wasichana mamlaka. Lakini wakati mwingine hata serikali hazitaki kuchukua hatua hii, aidha kwa kuwa hazioni umuhimu wake au kwa sababu za imani na mila potofu. Ripoti ya wataalamu inapendekeza maeneo manne yanayohitaji kuendelezwa ili kuwapa wasichana mamlaka:

- **Mazingira salama –** Wasichana wanahitaji mazingira wanayohisi ni salama kujieleza na ambapo wanaweza kujifunza na kucheza kadri ya matakwa yao. Haki ya kujifunza na haki ya kucheza zote zipo kwenye Sheria ya Haki za Mtoto (CRC).
- **Elimu na habari –** Elimu nzuri ni sehemu muhimu sana ya kupewa mamlaka, na shule zote ni lazima zijali mahitaji ya wasichana na kuwapatia mazingira salama ya kujifunza. Shule zinaweza pia kuwasaidia walimu na kuandaa vipaji vya kuwalinda na kuwasaidia wasichana. Kuwapa wasichana mamlaka pia inawezekana hata nje ya shule, kupitia mafunzo ya vitendo na kwa kushiriki katika vikundi na shughuli nyinginezo za vijana.

Tafakari
Unafikiri "mazingira salama" inapaswa iweje?

- **Kushiriki –** Inapasa wasichana waruhusiwe kushiriki katika maamuzi yanayoathiri maisha na hatima yao. Kushiriki inaweza kuwa ni moja ya namna nzuri zaidi ya

kuwapa mamlaka kwani inawafanya waweze kufikiri kupitia maswala na kuamua matokeo ya maamuzi yanayofanywa. Hata hivyo ni muhimu kushiriki ifanyike kwa jinsi watakavyo wasichana na siyo lazima kwa jinsi watakavyo watu wazima.

- **Mali Jamii** – Wasichana wengi hupata vipaji vya kijamii, hii ikiwa ni namna wanavyozungumza na kufanya kazi na jamii inayowazunguka, kupitia familia zao na shule. Hali inakuwaje kuhusu wasichana waliokosa bahati ya kuwa na familia na kwenda shule? Ni muhimu kutafuta njia za kuwaunganisha hawa wasichana na wanzao (marafiki wenye umri sawa na wao) ama washauri (wazee wenye uwezo wa kuwashauri) ambayo itamsaidia kila msichana kupata elimu jamii anayoihitaji.

Mapendekezo ya wataalamu

Serikali, mashirika ya kitaifa na ya kimataifa, na jamii kwa ujumla wanapaswa kufanya juu chini kuwapa wasichana mamlaka. Shule zina nafasi muhimu zaidi katika hili, na serikali zinapaswa kuhakikisha kuwa shule zina mahitaji za wasichana, ikiwa ni pamoja na fedha za kutosha. Vile vile, mambo yafuatayo yanaweza kutekelewa:

- Serikali zihakikishe kuwa elimu na huduma ya afya zinapatika bure kwa watoto.
- Wasichana wajengewe mazingira salama ili washiriki katika maamuzi muhimu.
- Mashirika yanayowatetea watoto wapewe fedha za kutosha.

> ***"Vijana wanaweza kuleta mabadiliko katika maisha yao. Mara nyingi tumetelekezwa, lakini sasa ni wakati mwafaka wa kusikiliza kilio chetu...."***
> ***Mwanamke*, mwenye umri wa miaka 20, Venezuela**

? Maswali ya kuyafikiria na kujibu:

- Tazama mikakati minne ya kuwapa wasichana mamlaka. Je, kuna mikakati mingine ya kuwapa wasichana mamlaka unayofikiri imeachwa? Kama ndiyo itaje na useme ina umuhimu gani?
- Kitu gani kingine kifanyike ili kuwapa wasichana mamlaka na nani anawajibika?

MASWALI YA KUYAFIKIRIA NA KUJIBU

Haya ni maswali yale yale yaliyoulizwa mwishoni mwa kila sehemu. Fikiria, yajadili na kisha tutumie majibu kabla ya tarehe **15 Januari 2007**. Unaweza kututumia majibu yako kwa njia yoyote kati ya tatu zifuatazo:

- **Tovuti**: Sauti za Vijana(http://www.unicef.org/voy/) kisha ingia "Zuia ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya wasichana" ili ujibu maswali yaliyioko kwenye mtandao.
- **Barua-pepe**: voy@unicef.org, ikiwa na kichwa cha habari "Zuia ubaguzi na ugandamizaji dhidi ya wasichana."
- **Barua**: Sauti za Vijana, 3 UN Plaza, New York City, NY 10017, USA.

? MASWALI

- Tazama orodha ya uvunjwaji wa haki za binadamu. Unafikiri kuna kitu kinachokosekana? Kama kipo, ungeongeza kipi na kipi unadhani ni muhimu?
- Ni nini kifanyike ili kuhakikisha sera na sheria zinatekelezwa na ni nani unafikiri anapaswa kuwajibika katika kuhakikisha haya yanatekelezwa?
- Tazama orodha ya sababu za ubaguzi na ukandamizaji. Unafikiri kuna kitu kinachokosekana? Kama kipo, ungeongeza kipi na kwa nini?
- Kitu gani kifanyike ili kuzuia ubaguzi na ukandamizaji wa wasichana na ni nani anapaswa kuwajibika ili kuhakikisha wasichana wanapata haki zao?
- Tazama orodha ya wasichana wenye matatizo. Unadhani kuna makundi yanayokosekana? Kama yapo, wewe ungeyaongeza yepi na kwanini unafikiri ni muhumu kufanya hivyo?
- Viongozi wa kijamii, vijana na wengineo wanawezaje kupata njia bora ya kuwalinda wasichana? Nani anapaswa kuhakikisha kuwa wasichana wanapata haki zao? Nani anapaswa kuwasaidia wasichana wenye shida?
- Tazama mikakati minne ya kuwapa wasichana mamlaka. Je, kuna mikakati mingine ya kuwapa wasichana mamlaka unayofikiri imeachwa? Kama ndiyo itaje na useme ina umuhimu gani?
- Kitu gani kingine kifanyike ili kuwapa wasichana mamlaka na nani anawajibika?

ASANTE!

***"Tunajukumu la kuwalinda watoto. Tunaweza kusaidia kuamua jinsi kizazi kijacho kitakavyokuwa."*- msichana mwenye umri wa miaka 16, Netherlands**

MAREJEO

- UNICEF, Voices of Youth, http://www.unicef.org/voy/discussions/.
- UNICEF, Voices of Youth, http://www.unicef.org/voy/explore/education/explore_166.html.
- UNICEF, Voices of Youth, 2006. "*Voices of Young People: Girls about Girls*" Prepared ahead of the expert group meeting in Florence, Italy in September 2006.
- Division for the Advancement of Women and UNICEF, 2006. "*Elimination of all forms of discrimination and violence against the girl child.*"
- United Nations Population Fund (UNFPA). 2005. "*State of World Population 2005.*"
- UNICEF, Youth Voices, http://www.unicef.org/voy/speakout/speakout_2655.html.

SISI NI NANI?

WGG: Kikundi Kinachoshugulikia Haki za Wasichana – Kikundi Kinachoishugulikia Haki za Wasichana ya Kamati ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya UNICEF na Mtandao wake wa kimataifa kuhusu Wasichana ni muungano wa Kamati za Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali yenye lengo la kuwafadhili wasichana, kwa hali na mali, popote pale walipo kupata haki zao za kibinadamu na kuwasaidia waweze kujiendeleza kimaisha.

VOY: Sauti za Vijana – Sauti za Vijana ni dirisha la tovuti iliyofunguliwa na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa kuhudumia Watoto UNICEF kwa ajili ya vijana wanaohitaji kufahamu zaidi, kufanya na kusema zaidi kuhusu dunia. Dirisha hili huwaunganisha watoto na vijana kutoka nchi zaidi ya 180 wenye nafasi ya kuchunguza, kujadili na kuchukua hatua dhidi ya maswala tete za haki za binadamu pamoja na maendeleo.